**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA**


**SHULE YA SEKONDARI**

# KORONA

S.L.P. 13402
ENGUTOTO – ARUSHA
Mkuu wa Shule +255757745774
Makamu Mkuu wa Shule +255768735043
Email: koronasecondaryschool@gmail.com


**KUMB. Na. KSS/ADM/JI/2022/01**

| |
|---|
| Bandika picha nusu (passport size) ya Wazazi/Walezi wakiwa pamoja na mtoto hapa |

**MZAZI/MLEZI WA:**
……………………………………
……………………………………

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023

1. Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022, tahasusi ya CBG au PCM. Shule ya Sekondari Korona ipo umbali wa kilometa 17.5 kutoka Arusha Mjini. Usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana Stendi ya kilombero na nauli ni Tshs. 500/=.kwa daladala zinazoelekea njiro atomic energy na teksi 20,000/=

2. Unatakiwa kufika shuleni Tarehe ambayo itatangazwa na TAMISEMI bila kukosa wala kuchelewa tayari kuanza masomo ya kidato cha TANO.

3. Muda wa kuripoti ni kabla ya saa kumi na mbili jioni, baada ya muda huo hautapokelewa.

4. Shule hii ni ya bweni kwa **Wavulana Pekee** wa kidato cha **Tano na Sita.**

## MAAGIZO YA KUTIMIZA KABLA YA KUFIKA SHULENI

1. Iwapo unakubali nafasi hii tafadhali jaza fomu zote zilizoambatanishwa na kusaini kila unapopaswa kisha uje nazo shuleni na kuzikabidhi kwa makamu mkuu wa shule.
2. '**Pay-in-slip** ya' Benki kwa uthibitisho wa malipo yote yaliyofanyika benki.
3. Nakala ya '**Result slip**' ya matokeo yako ya kidato cha nne.
4. Nakala ya cheti cha kuzaliwa kwa uthibitisho wa uraia.

## VIFAA/MAHITAJI YA LAZIMA UNAYOTAKIWA KULETA

1. Karo (ADA) ni Tsh. 35,000/= kwa muhula na Tsh. 70,000/= kwa mwaka. Ada hii ni muhimu ilipwe kwenye akaunti ya shule ya **NMB:** Jina **KORONA SECONDARY SCHOOL**, A/C No. **40801200307. N.B:** Pesa hazitapokelewa shuleni.

2. Godoro linapatikana shuleni kwa kulikodisha.

**MICHANGO MINGINE ILIPWE BENKI A/C No. 40801200306, NMB**

1. Kitambulisho Tsh. 5,000/=
2. Kuchangia malipo kwa wafanyakazi wasiolipwa na serikali Tsh. 60,000/= kwa mwaka.
3. Taaluma Tsh. 20,000/= kwa mwaka
4. Umiseta kwa mwaka 2000/=
5. Nembo ya shule Tsh. 2,000/=
6. Matibabu Tshs. 5,000/= (huduma ya kwanza)
7. Ukarabati Tshs. 10,000/= kwa mwaka
8. Vifaa vya maabara Tsh. 10,000/= kwa mwaka
9. Tahadhari Tsh. 2,000/= kwa mwaka

***Mwanafunzi ambaye hatakuja na pay-in-slip zinazoonyesha malipo aliyofanya benki hatapokelewa shuleni. Michango mingine yote isipokuwa ada haitapokelewa nusu****

***>>>>HAKIKISHA UNAINGIZA PESA KWENYE AKAUNTI SAHIHI<<<<***

**SARE YA SHULE** (Mwanafunzi Ajinunulie au anaweza kuzipata shuleni)

1. Mashati meupe mawili (2) ya mikono mirefu na isiyo na urembo wowote.
2. Suruali mbili za rangi ya ugoro iliyokolea (dark brown) upana wake iwe na uwezo wa kupanda gotini (isiwe myonyo)
3. Sweta rangi ya ugoro (dark brown).
4. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu. (Ajinunulie)
5. Tai rangi ya ugoro (dark brown), yenye mistari meupe
6. Soksi nyeusi jozi mbili
7. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia unifomu. (Ajinunulie)

**MAHITAJI MENGINE YA SHULE**

1. Rim mbili (2) za karatasi nyeupe (zisizo na mistari), mwanafunzi aje nazo siku ya kuripoti shuleni.
2. Nguo za michezo, raba nyeusi, bukta ya dark blue, T-shirt dark blue yenye kola. (Ajinunulie)
3. Track suit rangi ya maroon jozi mbili (2)
4. Shamba dress suruali ya dark blue upana wake iwe na uwezo wa kupanda gotini (isiwe myonyo) na iwe yenye pindo chini na t-shirt nyekundu yenye kola isiyo na maandishi wala mchanganyiko wa rangi nyingine yoyote. (Ajinunulie)
5. Shuka mbili rangi ya bluu zisizo na maua na Blanketi moja (1) zito. (Ajinunulie)
6. Chandarua nyeupe 1 ya duara na foronya 1 ya godoro la nchi mbili na nusu kwa futi sita, foronya 1 ya mto (rangi ya blue).
7. Sanduku Ia chuma lenye kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhia vifaa.
8. Bakuli, sahani, kikombe na kijiko (visiwe vya plastiki).
9. Ndoo 1 ya lita 20, Ndoo 1 lita 10 (zenye mifuniko); fagio 2 za chelewa; rubber squeezer 1; jembe kubwa 1; soft broom 1, hard broom 1, fyekeo 1, brashi 1 ya chooni yenye mkono mgumu kwa ajili ya usafi.
10. Madaftari ya kutosha (counter books - 4 quires) zisizopungua 8.
11. Scientific calculator (fx 991E-plus)1, mathematical set 1, Graph pad 2 na spring files 2
12. Dissecting kit 1 imara kwa wanafunzi wa Biolojia.

**VITABU:**

Ifuatayo ni orodha ya vitabu vinavyotumika darasani. Lazima mwanafunzi aje na angalau nakala moja kwa kila somo siku ya kuripoti shuleni.

| SOMO | ORODHA YA VITABU |
|---|---|
| 1. **ADVANCED MATHEMATICS** | • Advanced Level Pure Mathematics, fourth Edition by C.J Tranta<br>• Pure Mathematics I & II - J. K Backhouse<br>• S. Chand - Pure Mathematics class X1 and XII<br>• Understanding Mathematics – J. Thorn<br>• Advanced Level Mathematics - L.K. Shayo.<br>• Concise course for A'level statistics |
| 2. **BASIC APPLIED MATHEMATICS** | • Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools V and VI – Septine I. Sillem |
| 3. **PHYSICS** | • Principle of physics XI – S. Chand<br>• Principle of physics XII – S. Chand<br>• Understanding Physics - Jim Breclhaupt<br>• Objective of Physics – S. Chand<br>• Advance Physics - Roger Munchester<br>• Physics - Tom Duncan<br>• Calculation for A Level physics |
| 4. **CHEMISTRY** | • Conceptual chemistry XI and XII – S. Chand<br>• Advanced Inorganic Chemistry – Vol I and II – S. Chand<br>• Organic Chemistry Part A - Tanzania Publishing House<br>• Organic Chemistry Part B - Tanzania Publishing House<br>• Physical Chemistry – S. Chand<br>• Advanced Chemistry – Cambridge low price Edition Philip Mathew.<br>• A level Chemistry – 4th Edition EN |
| 5. **GEOGRAPHY** | • Landforms in Africa - Colin Buckle<br>• Principles of Physical Geography - Monkhouse<br>• Geography Integrated Approach - Waugh<br>• Practical Geography for Africa - J. M Pritchard<br>• Africa - J. M. Pritchard<br>• Tropical lands - Michael Seniar.<br>• Human and Economic Geography - Morgan.<br>• Geography dictionary<br>• Atlas of Tanzania<br>• The earth's physical environment, physical geography Alive - Zisti Kamili<br>• Advanced level Practical Geography Alive - Zisti Kamili |
| 6. **BIOLOGY** | • Biological science 4th edition - Taylor<br>• New understanding biology - Glenn & Suzan Toole<br>• Biology - S. Chand |
| 7. **GENERAL STUDIES** | • Understanding General Studies for Advanced Level: J.Bigirwamungu |

……………………

Mwl. CHRISTOPHER SABAS MALAMSHA

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KORONA

## MASHARTI YA KUZINGATIA KWA WANAFUNZI WOTE

1. Wanafunzi wote wanapaswa kufuata masharti, kanuni na sharia za shule.
2. Usafi wa bweni ni wajibu wa kila mwanafunzi anayeishi kwenye bweni.
3. Kila mwanafunzi anapaswa kushiriki utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na bustani za maua na mboga, usafi wa madarasa, mabweni, vyoo n.k.
4. Wanafunzi wote wanaapaswa kuheshimu na kufuata ratiba ya masomo ya darasani.
5. Kila mwanafunzi aheshimu na kutunza mali za shule, uharibifu wowote utakaotokea wa mali ya shule utagharamiwa na mwanafunzi mwenyewe.
6. Ugomvi wa maneno, matusi, kupigana ni mwiko.
7. Ruhusa zote za kulala nje ya shule zitatolewa na Mkuu wa shule au Makamu wake tu.
8. Mwanafunzi hatakiwi kubaki bwenini wakati wa masomo bila taarifa au ruhusa ya mwalimu wa zamu au patron.
9. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kutumia vyombo vya umeme kama vile heater, radio, pasi ya umeme, jiko ndani ya shule au kufanya ufundi wowote kwenye umeme ndani ya bweni na darasani.
10. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mwalimu au mfanyakazi asiye mwalimu bila ruhusa, kukaa jikoni au kujipikia.
11. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na vifaa vyenye ncha kali au vitu vinavyolipuka na dawa za aina zozote ndani ya bweni.
12. Siku ya kutembelea wanafunzi ni jumamosi ya kwanza ya mwezi kuanzia saa 7 mchana mpaka 10:00 jioni na wageni wote wataingia ofisi ya mwalimu wa zamu kabla ya kuonana na mwanafunzi. **Hairuhusiwi kuonana na mwanafunzi kabla ya kuonana na mwalimu**.

### (A) MAVAZI

I. Nguo za **binafsi (za nyumbani)** haziruhusiwi shuleni kabisa.

II. Wanafunzi wote wanatakiwa wavae sare husika za shule kwa wakati husika.

### (B) CHAKULA

I. Wanafunzi watapata chakula cha kawaida kufuatana na kiwango cha fedha kinachotolewa na serekali.

**(C) MATIBABU**

Taratibu za huduma ya kwanza zitapangwa na Mkuu wa shule pindi mwanao atakapojiunga na shule. Aidha endapo mwanafunzi ataugua **mzazi atagharamia** matibabu. Ili mzazi asiingie gharama kubwa tunashauri mzazi amkatie mwanae **BIMA YA AFYA** (Tsh. 50,400/= kwa mwaka) ambayo itamsaidia kwa mwaka mzima hata awapo nyumbani.

**JINA LA MWANAFUNZI: ..........................................................................**

**SAINI YA MWANAFUNZI............................ TAREHE............................**

**SAINI YA MZAZI / MLEZI ........................... TAREHE ............................**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na. 25 ya mwaka1978. Aidha, shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupata nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule.
3. Ni muhimu kuhudhuria na kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni (Preparation)
4. Kuwahi katika shughuli zote za shule na nyingine utakazopewa
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu juu ya wakati na muda sahihi wa kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa mwanafunzi katika shule hii.
6. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
7. Kuvaa sare za shule wakati wote kwa mujibu wa taratibu na kanuni za shule.
8. Kuzingatia Ratiba ya shule wakati wote.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUWA SHULE

1. Wizi
2. Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 99 bila taarifa/utoro
3. Kugoma na kuhamasisha mgamo
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga/kutishia kampiga mwalimu au mtu veyote yule.
6. Ulevi au unywaji wa pombe.
7. Uvutaji wa sigara, bangi na matumizi ya madawa ya kulevya au kukutwa na vitu hivyo shuleni au nje ya shule.
8. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja.
9. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
10. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
11. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au laini va simu katika mazingira ya shule.
12. Kudharau bendera ya Taifa.
13. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
14. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
15. Kutoroka shule katika siku za masomo.
16. Kutokuvaa sare ya shule.

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII

**1.** Mimi……………………………………………….(Jina kamili la **mwanafunzi**), Kidato cha………….. mwaka ……….. natambua wajibu wangu kama mwanafunzi kwa Taifa na jamii kwa ujumla na ninaahidi kwamba:

A. Nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
B. Nitatii na kuheshimu viongozi wangu wote kuanzia viongozi wa darasa, viranja, watumishi wote wasio walimu na walimu hadi mkuu wa shule.
C. Sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wote nitakapokuwa shuleni labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali kwa maandishi kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe.
D. Sitagoma wala kusababisha mgomo wowote kwa kipindi chote nitakapokuwa nikisoma katika shule hii.
E. Kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu, hatua kali za nidhamu zichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

……………………………………… ………………………… ……………
JINA KAMILI SAINI YA MWANAFUNZI TAREHE

**2.** Mimi …………………………………………………………………… **Mzazi / Mlezi**

wa ……………………………………………………………………………………………

Nimesoma na kuelewa /kukubaliana na sheria na kanuni za shule. Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masorno au kufukuzwa shule.

Pia nitakuwa mwaminifu kutoa ada na michango yote iliyokubaliwa kisheria bila usumbufu na kuhakikisha mtoto wangu anapata mahitaji yote ya muhimu.

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………..

……………………………………… ………………………… ……………
JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI SAINI YA MZAZI/MLEZI TAREHE

**3.** Mimi ………………………………………………………… (Jina la **mwenyekiti wa mtaa/kijiji)**, Mwenyekiti wa mtaa/kijiji cha ………………………………………… nathibitisha kuwa Ndugu ……………………………………………………………… ni Mzazi/mlezi wa mtoto huyu aliyechaguliwa kujiunga kidato cha tano.

Maoni/mapendekezo kuhusiana na unavyomfahamu mwanafunzi huyu: ………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

MUHURI

NAMBA YA SIMU ……………………

………………………………………… ……………………

SAINI YA M/KITI (KIJIJI/MTAA) TAREHE

**4.** Jina la **Mtendaji Kata** ……………………………………………………………………

Kata ya …………………………

MUHURI

NAMBA YA SIMU ……………………

………………………………………… ……………………

SAINI YA MTENDAJI KATA TAREHE

KORONA SEC SCHOOL
Education for Better Life

**HABARI ZA MZAZI / MLEZI**

Tafadhali taarifa hizi ni za muhimu sana zijazwe kwa usahihi

1. Jina kamili Ia Baba …………………………………………………………………
2. Kazi yake……………………………………………………………………………
3. Anwani ya mahali pa kazi ya baba ………………………………………………
   Namba ya simu…………………………………………………………………………
4. Jina kamili la Mama…………………………………………………………………
5. Kazi yake……………………………………………………………………………
6. Anwani ya mahali pa kazi ya mama………………………………………………
   Namba ya simu…………………………………………………………………………
7. Jina kamili Ia Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)

   ……………………………………………………………………………………………
8. Kazi na anwani ya mIezi
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
9. Nyumbani kwa Baba (alipozaliwa mtoto) Kijiji /Mtaa…………………………

   Wilaya………………………………… Tarafa ……………………………………

   Kata……………………………………… Mkoa ……………………………………
10. Mtoto anaishi na
    I. Baba tu ☐
    II. Mama tu ☐
    III. Wazazi wote ☐ (*weka alama yay a vema*)
    IV. Walezi ☐
11. Dini ya baba …………………………… Dhehebu ………………………
    Dini ya mama …………………………… Dhehebu ………………………
    Dhehebu unalotaka mwanao alelewe ……………………………………………
12. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo
    ……………………………………………………………………………………………
13. Mimi …………………………………………… (Jina la Baba/Mama/Mlezi) wa ………………………………………… nathibitisha kuwa taarifa hii hapa juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu na uongozi wa shule ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

……………………………………… ……………………… ……………

**JINA KAMILI** **SAINI** **TAREHE**

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a medical Officer in Government Hospital in respect of all entrants to Korona Secondary School)

Pupil's full name ……………………………………………………………………………

Age ……………………………………………………………………………

1. Blood count (red and white) ………………………………………………………
2. Stool examinations ………………………………………………………………
3. Urinalysis ………………………………………………………………………
4. Syphilis test ………………………………………………………………………
5. T.B. test …………………………………………………………………………
6. Eye test …………………………………………………………………………
7. Ears test …………………………………………………………………………
8. Chest ……………………………………………………………………………
9. Abdomen ………………………………………………………………………
10. Spleen……………………………………………………………………………
11. Additional information: e.g. physical defect, infection, chronic or family diseases etc
    ………………………………………………………………………………………
    ………………………………………………………………………………………
    ………………………………………………………………………………………
    ………………………………………………………………………………………
    Treatment after examination
    ………………………………………………………………………………………
    ………………………………………………………………………………………
    ………………………………………………………………………………………
    ………………………………………………………………………………………
    (Please state nature of treatment)

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further studies

Signature ………………………………………

Designation ……………………………………

Station …………………………………………

Date: …………………………………………

Official stamp …………………………………